MOTO WA MABADILIKO UMEANZA...

Cheche za Fikra

JUZUU 3 TOLEO 10

OCTOBA 22, 2008

KIJARIDA CHA BURE— UKISHASOMA MPE MWINGINE—USIBANIE!

VIFO VYA WATOTO TABORA

RIPOTI YAPENDEKEZA NSSF IWAJIBISHWE



Jengo ambalo NSSF Ilizembea kuwajibika

Na. Fred Katunzi



Kile ambacho "Cheche" ilithubutu kukisema muda mfupi baada ya taarifa za vifo vya watoto 19 Tabora kimeonekana kuwa ni kweli.

Hatimaye ushahidi umewekwa wazi kuwa NSSF inastahili kubebeshwa lawama za kutosha kabisa kwa kutokea vifo vya watoto 19 na mipango ifanywe ili shirika hilo lifikishwe mahakamani kwa kesi ya madai kutokana na ukiukwaji mkubwa wa taratibu, uzembe na kutokujali kulikosababisha vifo vya watoto hawa.

Tume iliyochunguza tukio hilo na iliyoongozwa na Mkuu wa Polisi wa Mkoa wa Tabora Bw. Mmari imesema katika muhtasari wake kuwa "Siku ya tarehe 01/10/2008 kumbi za 'Bubbles Club' na NSSF (110 Disco Theque) zilijaza watu wengi kupita uwezo wake kwa lengo la kupata mapato zaidi. Ulikuwepo mbanano mkubwa ndani ya kumbi hizo, joto kali na haikuwepo nafasi ya kutoshaya kucheza mziki." Zaidi ya yote kwa mujibu wa ripoti hiyo "Joto kali ndani ya ukumbi wa Bubbles Club' ilisababishwa na msongamano mkubwa wa watu,kushindwa kufanya kazi kwa viyoyozi, kukosekana kwa mzunguko wa hewa safi, uvutaji sigara ndani ya ukumbi, unywaji pombe na rangi iliyokuwa imepakwa siku chache kabla ya siku hiyo kulisababisha watoke jasho, wasikie kiu, harufu mbaya na kukosa hewa safi hali iliyowafanya watoto kutafuta njia ya kutoka ndani ya ukumbi."

NSSF inastahili kubebeshwa lawama!

Ripoti hiyo yenye kurasa karibu mia moja na vielelezo kadhaa imeonesha kile ambacho kijarida chako cha Cheche kiliweza kukionesha mara moja kuwa Shirika la Hifadhi ya Jamii la Taifa (NSSF) linawajibika moja kwa moja katika kutokea vifo vya watoto hawa. Ripoti hiyo pia inagawanya kuwajibika huko pia kwa watu na taasisi mbalimbali lakini pasipo shaka yoyote inaonesha ni jinsi gani NSSF kwa kutafuta faida kwa namna yeyote iliruhusu uchezeshaji madisko kwenye jengo lake ilhali ikijua au ilipaswa kujua kuwa makampuni hayo hayakuwa na vibali vya kufanya biashara ya sanaa.

(Inaendelea Uk 2)



Benjamin. G. Mwalukasa

Kijarida Ulichoshika

- **Kinatoka kila Jumanne**
- **Ni cha bure kabisa!**
- **Kisichofungamana na chama chochote au fisadi yeyote!**
- **Kiko huru, kinathubutu, na hakiogopi mtu au hoja yoyote.**
- **Ni kijarida chako!**
- **Haki zote za kuchapa na kunakili zimeruhusiwa!**

HOJA YA MWANAKIJIJI — NYONI NA DAU WAWAJIBISHWE!

Kama kulikuwa na utata juu ya nafasi ya Shirika la Hifadhi ya Jamii la Taifa (NSSF) kwenye vifo vya watoto 19 na majeruhi wengine karibu idadi hiyo hiyo utata huo sasa haupo tena.

Tume iliyoundwa kuchunguza suala hilo imeonesha pasipo shaka yoyote kuwa Shirika hilo lenye mabilioni ya fedha za wafanyakazi wa Tanzania limeonesha uzembe, kujali faida, na kutofuata taratibu kiasi cha kuruhusu majengo yake kutumiwa kinyume cha makusudio yake.

Kwanza kwa kuruhusu majengo yake yatumiwe kwa shughuli za sanaa kinyume na mkataba na pili kuruhusu shughuli ambayo haina kibali kufanyika kwenye majengo yake.

Ni wazi kuwa ripoti hii ni ushahidi wa kutosha kuwawajibisha Mwenyekiti wa Bodi ya shirika hilo Bi. Blandina Nyoni na Mkurugenzi wake Dr. Ramadhani Dau kutokana na uzembe, kutokuwajibika, na ukiukaji taratibu.

Ndani ya Toleo Hili

NSSF yahusika	1, 2
Wawajibishwe!	1
Alama za Nyakati?	2
Mikwara ya Kikwete	3
Ujenzi bila viwango?	3
Maoni ya Mtandao	4
Picha na Katuni	4

HABARI MBALIMBALI

WANASOMA ALAMA ZA NYAKATI?

Na. Mahmoud Rashid



Mojawapo ya vitu ambavyo vimenishangaza sana ni kitendo cha wananchi wa kijiji cha Kanga uko Chunya kufanya kile ambacho hakijawahi kufanywa katika historia ya nchi yetu nacho ni kuutupia mawe msafara wa Rais.

Ingawa Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Ikulu Bw. Salva Rweyemamu amesema kuwa magari yaliyotupiwa mawe hayakuwa kwenye msafara "wenyewe" wa Rais ukweli unabakia kuwa magari hayo yalikuwa ya serikali na ambayo yalikuwa huko kutokana na ziara ya Rais na hivyo ni haki kabisa kuyataja kuwa ni ya "msafara wa Rais".

Kitendo cha kurushiwa mawe ni cha kihalifu si kwa sababu kimetokea kwenye ziara ya Rais bali ni kwa sababu ni ishara ya uhuni na mtu kushindwa hoja.

Lakini ni kitendo kile kile kilichotokea Tarime ambapo Mchungaji Mtikila alijikuta akijeruhiwa katika mojawapo ya kampeni za kisiasa.

Ninachoona ni kuwa hizi ni alama za Nyakati!

Lakini hili linapotokea katika ziara muhimu kama hii ambayo ilikuwa inasubiriwa kwa hamu itakuwa ni kudharaua Watanzania kulifanya jambo hili ni dogo na watu "wasilikuze". Na itakuwa ni kosa kubwa kulaumu vyombo vya habari kana kwamba serikali ndiyo ina ukiritimba wa habari za ukweli.

Ninachoona ni kuwa hizi ni alama za nyakati. Walianza kuzomewa, kubebewa mabango na sasa kupopolewa kwa mawe.

Naamini wakati umefika wa kujiuliza CCM imepotoka wapi? Je serikali imekwenda wapi kombo? Siyo mara ya kwanza kwa kiongozi kushindwa kusimama mahali au kuhututubia. Lakini imekuwa ni mara ya kwanza kwa msafara kupigwa mawe.

Je ni ishara kuwa watu wamechoka kuahidiwa na kupewa maneno matamu? Yawezekana ni ishara ya nyakati mpya?

RIPOTI VIFO VYA WATOTO (KUTOKA 1)

Licha ya ripoti hiyo kuwa ya kujipendelea (haimuwajibishi Mkuu wa Mkoa wala Mkuu wa Polisi) imeweza kuwanyoshea kidole watu wengine lakini ni wazi kidole cha kwanza kimeelekezwa kwa NSSF.

"Usanifu wa ngazi la jengo la NSSF uliziingatia matumizi ya kiofisi na si kwa kupitisha watu wengi kwa wakati mmoja.Mapungufu hayo ya ngazi yalikwamisha kupitia watu wengi kwa wakati mmoja hivyo kuchangia tukio la vifo vya watoto19." Inasema ripoti hiyo. Kwa mujibu wa ripoti hiyo hiyo makampuni yaliyoendesha madisko hayo ya watoto hayakuwa na vibali vya kufanya hivyo. "'Bubbles Club' haikuwa na usajili hai wa BASATA hivyo haikustahili kupewa kibali chochote cha kuendesha shughuli za sanaa. Na "110 Disco Theque' haina usajili wa BASATA hivyo haikustahili kupewa kibali cha kkuendesha shughuli za sanaa."
Kwa maneno mengine NSSF iliruhusu majengo yake yatumike kufanya shughuli isiyo halali. Kauli inayoishtaki NSSF ni sehemu mbili ambapo inasemwa kwanza kuwa "Matumizi yliokusudiwa na mmiliki wa jingo la NSSF kwa kumbi za '110 Disco Theque' na 'Bubbles Club' ni kwa mikutano na sherehe za kiofisi (Functional Hall/ Meeting). Mkataba hai wa upangaji kati ya NSSF na Manji L. Patel(Bubbles Club) ni kwa matumizi ya ofisi." Hivyo inasemwa wazi kabisa NSSF ilijua jengo lake ni kwa ajili ya shughuli za Ofisi na ndivyo mkataba unavyosema .

Lakini ripoti hiyo inaongezea na kusema kuwa licha ya NSSF kujua kuwa jengo hilo ni kwa ajili ya shughuli za kiofisi "uongozi wa NSSF unakiri kuwa ulifahamu kuwa Manji L. Patel aliomba ukumbi huo kwa lengo la kupiga Disco na kwamba kosa lililofanyika ni katika kujaza mkataba (Typographical error)."

Ripoti hiyo ambayo ilikuwa inasubiriwa kwa hamu inaonesha nafasi ya NSSF katika kusababisha vifo vya watoto hawa na kujeruhi wengine pale ambapo "uongozi wa NSSF ulifahamu na ulitoa kibali cha mabadiliko yaliyofanywa na mmiliki wa 'Bubbles Club'ya kuziba madirisha na sehemu nyingine za kupitisha hewa ya asili pamoja na hatua ya kuufanya ukumbi huo upitishe sauti (sound proof)."

Hili ni jambo muhimu kwani katika kuelezea sababu ya vifo vya watoto hawa ripoti inasema kuwa "taarifa ya uchunguzi wa kitaalam imeonyesha kuwa watoto hao walifariki kwa kukosa hewa safi". Kwa maneno mengine kitendo cha NSSF kuridhia kubadilisha ukumbi huo kutoka matumizi ya ofisi na kuufanya ukumbi wa disko pamoja na kuridhia kuziba madirisha na milango ya dharura kunafanya shirika hilo kuwa mshiriki wa moja kwa moja wa tukio hilo la kuhuzunisha.

Ripoti inaendelea kuikamata NSSF kwa kusema kuwa "Pamoja na jambo hilo, hawakumtaka mpangaji huyu kuwapatia michoro ya marekebisho hayo ili waiwasilishe kwa mhandisi wa Manispaa kuomba kibali cha ujenzi. Kutokana na kutozingatiwa kwa taratibu, mmiliki wa 'Bubbles Club' alifanya mabadiliko ambayo hayakuzingatia ushauri wa kitaalamu na tahadhari za kiusalama kama vile kuwa na milango zaidi ya dharura (escape routes) na vifaa vya kugundua moto (smoke and heat detectors)"

Hivi karibuni Mkurugenzi wa NSSF Dr. Ramadhani Dau amejaribu kuelekeza mawazo ya watanzania kwenye anachoamini ni mafanikio ya NSSF katika ujenzi wa majengo mbalimbali na kukwepa kuzungumzia kuwajibika kwenye fivo vya watoto hawa.

Wananchi wengi wanasubiri kuona kama serikali ya Rais Kikwete itathubutu kuwachukuklia hatua NSSF taasisi inayoongozwa na swahiba wake wa karibu.

MPATIE MTU MWINGINE BURE

NGUVU ZA HOJA

BILA VIWANGO BORA TUTAANGAMIA

Na. Dr. Bertha Maegga

Nashukuru kusoma habari za maafa yaliyowapata watoto wetu katika nakala ya Cheche za Fikra, Juzuu 3 toleo 8 la Oktoba7, 2008.

Ijapokuwa ni habari ya kusikitisha, lakini kujua kwamba kuna wanaojali kuchukua hatua za tahadhari kwa matukio ya namna hiyo baadaye ni faraja.

Sasa sijui hatua hizo zitaishia katika mazungumzoau zinaweza kusogea mbele zaidi kuingia katika harakati na kampeni ya nguvu ili kushinikiza hatua madhubuti, za uhakika zichukuliwe ili matukio hatarishi kama hayo yasitokee mara nyingine.

Ni matukio yanayoweza kuzuilika, lakini yanahitaji kufanyiwa kazi kwa nguvu na ya kudumu kwa muda mrefu ili wenye madaraka ya uamuzi na wenye uwezo wa kuibadili hiyo hali wasikie, wasukumwe kuyafanyia kazi inayoeleweka.

Zaidi ya hayo, matukio ya kiuzembe yanayoleta maafa si hayo tu, yako mengi. Unaweza kurejea katika kumbukumbu zako, kwamba kuna vingine vimeshatokea katika nyumba za kulala vijana wa shule mbalimbali, nchini Tanzania na hata kwa jirani zetu, ambapo bweni linaungua, na watoto wanteketezwa pamoja na mali zao au wenyewe wanapona chupuchupu, lakini vyote walivyo navyo vinateketea.

Umma haupati taarifa halisi ya sababu zilizowezesha matukio kama hayo yatokee, na hatua za kuzuia yasitokee tena hapo na mahali pengine.

Kwa hali hiyo, pamoja na ushauri wa kuwajibika kujifunza na kutumia CPR Cheche ilivyoshauri, kuna kazi kubwa zaidi ya kufanya, kama kweli tunataka kuwajibishana. Swala zima la viwango vya usalama katika miundo mbinu yetu mingi haijatiliwa maanani kabisa. Hii ni pamoja na ujenzi wa nyumba za kuishi sisi wenyewe. Je viwango vya nyumba za kuishi, nyumba za kufanyia kazi / biashara, na hata hizo za starehe zina viwango vinavyokidhi mahitaji ya usalama wa watumiaji?

Kwenye "Cheche za Fikra", pengine mnaweza kutafiti zaidi ukubwa wa tatizo hili, ambalo linamgusa kila mtu. Usalama wa mmoja ukiwa hatarini, ni usalama wa mtaa mzima na jamii inayoishi jirani.

Sidhani kama tuna viwango na vipimo vya usalama katika sehemu mbalimbali ya miundo mbinu yetu. Tunahitaji la haraka kuwa navyo.

Hatuna budi kufanya kila jitihada kuweza kuwa na viwango vya namna hiyo ambavyo vitaweza kulazimishwa kisheria. Vinginevyo maisha ya kwenye miji yetu ni ya hatari zaidi kuliko kuishi katika misitu ya Congo au ile ya Amazoni.

Dr. Bertha Maegga, PhD., ni Mtafiti Mkuu katika Taasisi ya Taifa ya Utafiti iliyoko Ocean Road Jijini Dar-es-Salaam.

HUKUMU YA KIFO HAIMTISHI MUUAJI

Na. Jessy L. Fundi



Nilikuwepo kwenye maandamano ya kupinga mauaji ya Albino yanayoendelea nchini. Nilikuwa nimerejea tu kutoka kijijini ambako kulikuwa na habari zilizokuwa zikienea kuwa kuna mtoto mwingine Albino ameuawa kinyama kwa sababu tu ya ulemavu wake.

Nilipokaa kumsikiliza Rais nilijikuta nimeshikwa na donge moyoni. Rais Kikwete haelewi hata kidogo uzito wa suala hili na kama anaelewa basi hana kusudio la dhati la kukabiliana na uhalifu huu.

Hakuna mahali popote duniani ambapo adhabu ya kifo peke yake imeonesha kupunguza mauaji ya watu wengine.

Mtu anayeamua kuua kwa makusudi ameshapima faida na hasara na ameona faida inazidi hasara. Kwa kadiri ya kwamba faida kubwa inaahidiwa kwa kupata viungo vya Albino basi watu wataendelea kujaribi kufanya hivyo licha ya kujua kuwa adhabu yao (wakikamatwa na kushughulikiwa kisheria) ni kifo.

Ni kwa sababu hiyo natoa wito wa uongozi wa serikali kukaa chini na kufanya tathmini ya kweli ya kukabiliana na wimbi la mauaji haya. Kwa sababu motisha wa mauaji haya ni fedha, nashangazwa kwanini hakuna dau la nguvu lenye kushawishi watu kuwasaliti waganga wa kienyeji na wanaofanya mauaji haya? Kweli kuna ugumu wa serikali kutoa dau la pesa ya kuvutia kwa mtu yeyote atakayewezesha kupatikana, kushtakiwa na hatimaye kukutwa hatia kwa wanaohusika na uharamia huu?

Jinsi suala hili linavyoshughulikiwa ni kana kwamba hatuna vyombo vya usalama. Hivi sisi kama Taifa tunaweza vipi kupata usingizi usiku huku tukijua kuwa kuna wenzetu ambao wanawindwa kama swala?

Rais Kikwete, Waziri Mkuu, Mkuu wa Jeshi la Polisi na vyombo vingine vya usalama wanapata wapi ujasiri wa kutembea na suti zao wakati wana na mabinti wa Taifa hili wanauawa kama wanyama wa mawindo?

Kwanini hatujaona makanisa, misikiti, na asasi nyingine kufanya maandamano makubwa kabisa katika historia ya nchi yetu kupinga mauaji haya na kuonesha kuchukizwa na ubutu wa serikali?

Kwanini hadi leo tumeshindwa hata kutoa dau la Shilingi milioni 10 kwa yeyote atakayefanikisha kukamatwa kwa wauaji hawa? Tumebakia kupigana mikwara majukwaani? Ole wetu kutokana na ukimya na ubutu wa vitendo vyetu.

Watanzania zaidi ya 30 wameuawa kinyama na sisi bado tunacheka cheka na kurembuliana macho? Wamekufa watoto 19 kiuzembe na bado tunapiga makofi kuwashangilia watawala? Tumelaaniwa!

Soma bure


MOTO WA MABADILIKO UMEANZA...


KATUNI ZA WIKI

Picha za Wiki



Tupige vita mauaji ya ndugu zetu Albino!







KUTOKA KWENYE MTANDAO

Napenda kuwahakikishia kuwa pale palipojitokeza tukio hilo tulichukua hatua na kama kutatokea Albino kufanyiwa vitendo vya kubaguliwa popote pale tupeni taarifa na hatua zipasazo zitachukuliwa dhidi ya wahusika.- **Rais Kikwete** (Masaa machache baadaye kulikuwa na taarifa ya Maalbino wawili kuuawa)

Raisi wa nchi akiwa dhaifu kiutendaji ndani ya nchi huwa ni mzigo mkubwa usiobebeka kwa vyombo vya ulinzi na usalama.Kutwa wanakuwa wakikimbizana kama vichaa huku na huko na waitwao adui wa Raisi badala ya kushughulikia mambo mengine.— **Netanyahu**

Taarifa hii inalenga kuweka bayana ukweli ulivyokuwa katika ziara hiyo ambako, kwa mara nyingine, Rais alipata nafasi nyingine nzuri ya kufanya kile ambacho hukifurahia sana kukifanya, yaani kukutana na wananchi, kusikiliza kero zao, karaha zao, raha zao, mafanikio yao, na mahitaji yao ambayo wanaamini Rais wao anaweza kusaidia kuyatafutia majawabu.—**Ikulu**

Ni vyema ikakumbukwa kuwa uchunguzi unaofanywa na SFO siyo kwa ajili ya Tanzania bali ni kwa ajili yao wenyewe na kampuni yao ya British aeroscope. hivyo Serikali itakachosema ni kwamba Uchunguzi wa SFO ilikuwa ni kwa ajili ya waingereza wenyewe na Kampuni yao. Hivyo Serikali baada ya kupata report ya uchunguzi watajidai kuwa wanaitisha uchunguzi mwingine sasa. Uchunguzi utaendelea weeeeeee mpaka mtasahau. Kama ilivyotokea kwa Richmond— **Mpiganajinamba moja**

Mkapa haitaji hizo zawadi. alikwisha jilipa mwenyewe mara kadhaa hizo. Katika himaya ya yamafisadi kila mmoja anajilipa kadriya madaraka yake. Mo asipoteze wakati wake kuanagalia Afrika Mashariki. Huku kazi moja tu! Kukupua kila nafasi inapotokea. Huku Wizi ni halali.— **Mchora**
(baada ya kufika taarifa kuwa Rais Mkapa hakupata tuzo ya Mo' ya Utawala Bora Afrika)

MPATIE MTU MWINGINE BURE

Cheche za Fikra
Mchapishaji na Mhariri Mtendaji

M. M. Mwanakijiji

Timu ya Waandishi
Benjamin Mwalukasa— Mhariri

Freddy Katunzi—Habari za Siasa

Mahmoud Rashid—Habari mbalimbali

Jessica L. Fundi – Makala

Kwa kujiandikisha,
maoni, habari, na ushauri

Tuandikie: Mhariri@klhnews.com

Tembelea: http://www.klhnews.com

Kanusho: ***Mawazo yanayonukuliwa hayawakilishi msimamo au mawazo ya mchapishaji na utawala wa kijarida hiki.***